



GRETSA UNIVERSITY - THIKA

UNIVERSITY EXAMINATIONS MAY - AUGUST 2023 SEMESTER

BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

KODI: KISW 301

KOZI: SINTAKSIA NA SEMANTIKA YA KISWAHILI

TAREHE: 1 AUGUST 2023

WAKATI: 8:00 AM - 11:00 AM

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MATATU**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. **ANDIKA VIDOKEZO VYAKO NYUMA YA KIJITABU CHA MAJIBU KISHA PIGIA MSTARI BAADAYE**

TAHADHARI:-kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani

SEHEMU YA A: YA LAZIMA

SWALI LA KWANZA

- a) Zichanganue sentensi zifuatazo ukitumia vielelezo matawi:
- i. Mwachilumo anaimba wimbo mtamu kanisani. [Alama 4]
 - ii. Kamau na mke wake mpole wamenunua ardhi kwa bei ghali. [Alama 6]
 - iii. Viongozi tuliwachagua wametuongezea mzigo wa ushuru. [Alama 4]
- b) Bainisha mambo yoyote matatu yanayoshughulikiwa katika sintaksia. [Alama 3]
- c) Dhihirisha mapungufu yoyote mawili ya Nadharia ya Sarufi Mapokeo. [Alama 2]
- d) Itaje misingi yoyote mitano ya Nadharia ya Sarufi Muundo [Alama 5]
- e) Huku ukitaja mifano, jadili aina zozote nne za maana. [Alama 12]
- f) Zifafanue dhana zifuatazo:
- i. Upole [Alama 2]
 - ii. Vitendo usemi [Alama 2]

SEHEMU YA B: YAJIBU MASWALI YOYOTE MATATU

SWALI LA PILI

- a) Kwa kutumia mifano, yafafanue mahusiano yafiatayo ya kifahiwa katika ya maneno ya Kiswahili Sanifu:
- i. Sinonimi [Alama 4]
 - ii. Polisemi [Alama 4]
 - iii. Homonimi [Alama 4]
- b) Bainisha vijumlishwa vitatu vitatu vya sentensi zifuatazo:
- i. Chausiku anaandaa kishuka. [Alama 3]
 - ii. Ndweo anajenga nyumba nzuri. [Alama 3]
- c) Eleza dhana ya usonde. [Alama 2]

SWALI LA TATU

- a) Fafanua kategoria zozote nne za kisarufi. [Alama 12]
- b) Dhihirisha miundo yoyote minne ya Kirai Nomino cha Kiswahili Sanifu. [Alama 8]

SWALI LA NNE

- a) Ichanganue sentensi ifuatayo kwa kutumia uchanganuzi kiuambajengo. [Alama 4]
Mwalimu wetu anametufunza somo hili vizuri.
- b) Bainisha mapungufu mawili ya uchanganuzi kiuambajengo. [Alama 2]
- c) Kwa kutumia mfano, dhihirisha namna geuzi la ukanushaji linavyoweza kutokea katika sentensi za Kiswahili. [Alama 8]
- d) Eleza michango mitatu ya Nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo. [Alama 6]

SWALI LA TANO

- a) Huku ukitumia mifano katika sentensi, zifafanue kategoria amilifu zifuatazo katika Kiswahili Sanifu:
- i. Kiima [Alama 3]
 - ii. Kiarifu [Alama 3]
 - iii. Kijalizo [Alama 3]
 - iv. Yambwa [Alama 3]
- b) Kwa kutaja mifano, jadili dhana ya uchukulizi katika Kiswahili Sanifu. [Alama 8]